**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI

NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 2330

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I-II

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

ISBN: 978-9912-9958-5-7

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 4 Mei 2026 kuwa Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I-II nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU ELIMU YA AWALI NA MSINGI DARASA LA I-II

**2026**

© Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (TISTA), 2026

Toleo la Kwanza, 2026

ISBN: 978 - 9912 - 9958 - 5 - 7

Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (TISTA)

S.L.P 55104,

Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 784 267 762

Barua pepe: islamicstudies@tista.or.tz

Tovuti: www.tista.or.tz

Umechapishwa na:

Taasisi ya Elimu Tanzania

Muhtasari huu urejelewe kama : Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (2026*), Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I-II.* Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (TISTA)

# Yaliyomo

Orodha ya majedwali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .iv

Vifupisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . v

Shukrani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .vi

1.0 Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

3.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi, Mzazi/Mlezi na Jamii katika Ufundishaji na Ujifunzaji. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 2

3.1 Mwalimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 2

3.2 Mwanafunzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 2

3.3 Mzazi/Mlezi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

3.4 Jamii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

4.0 Malengo ya Elimu ya Awali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

5.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I na la II . . . . . . . . . . . . . . . . . 4

6.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Awali. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 4

7.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II. . . . . . . . . . . . . 4

8.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Elimu ya Awali . . . . . . . . . . . . 5

9.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Darasa la I na la II . . . . . . . . . . 5

10.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

11.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

12.0 Upimaji. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

13.0 Muda wa Kufundisha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7

14.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9

Elimu ya Awali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 10

Darasa la I . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 13

Darasa la II . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 16

Bibliografia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 19

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Elimu ya Awali ............... 5

Jedwali Na:2 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la I-II .................. 5

Jedwali Na:3 Mgawanyo wa vipindi kwa Elimu ya Awali ..................................... 7

Jedwali Na.4 Mgawanyo wa Vipindi kwa Darasa la I ............................................ 8

Jedwali Na.5 Mgawanyo wa Vipindi kwa Darasa la II ............................................ 9

Jedwali Na.6 Maudhui ya Elimu ya Awali ..............................................................10

Jedwali Na. 7 Maudhui ya Darasa la 1 .................................................................... 12

Jedwali Na. 8 Maudhui ya Darasa la II .................................................................. 16

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TISTA | Tanzania Islamic Studies Teaching Association |

**Shukurani**

Kila sifa njema anastahiki Allah (*subhaanahu Wata'ala*) Mola Mlezi wa viumbe vyote. Rehema na amani zimuendee Mtume wetu Muhammad (*Swallallaahu'Alayhi Wasallam*), Maswahaba zake pamoja na wafuasi wake wote.

Maandalizi ya Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I-II yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za Kiislamu. Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (TISTA) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Wataalamu hawa wamefanya kazi kwa weledi mkubwa kuhakikisha kuwa maudhui ya muhutasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kuishi maisha yenye maadili mema na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la Uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TISTA inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Sheikh, Dkt.Abubakar Zubeir Bin Ally Mbwana

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania

**Kiongozi Mkuu**

**Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Elimu ya Dini ya Kiislamu ni somo la lazima kwa wanafunzi waislamu wa ngazi ya Elimu ya awali na Msingi Darasa la I na la II nchini**.** Lengo la kufundisha somo hili ni kumjenga mtoto awe mcha Mungu na muadilifu katika maisha yake. Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I–II, Tanzania Bara. Aidha, muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023 ambao msingi wake mkuu umejikita kupata wahitimu wenye maarifa, maadili, uadilifu, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kumudu maisha yao ya kila siku.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya Elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi, Mzazi/Mlezi na Jamii katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji na unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi na jamii katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 3.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa;

(b) Kuandaa mazingira salama, rafiki na wezeshi ya kufundishia na kujifunzia;

(c) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(d) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji;

(e) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo;

(g) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika malezi na ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 3.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa;

(c) Kushirikiana na wenzake pamoja na mwalimu katika mchakato wa ujifunzaji; na

(d) Kuzingatia kanuni na taratibu za shule.

### 3.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji;

(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) Kufuatilia mwenendo wa kitabia wa mwanafunzi;

(d) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(e) Kumpatia mwanafunzi vifaa vinavyotumika katika shughuli ya ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji muhimu;

(g) Kumfundisha mtoto umuhimu na thamani ya elimu na kazi pamoja na kumuhimiza kujifunza kwa bidii;na

(h) Kumsimamia mtoto atekeleze ibada akiwa nyumbani

### 3.4 Jamii

Jamii inatarajiwa:

(a) Kutoa fursa kwa mtoto kujifunza mambo yenye manufaa kwa maisha yake ya dunia na akhera.

(b) Kuandaa mazingira wezeshi kwa mtoto kujifunza tunu zilizohifadhi utambulisho na utu wake

(c) Kushirikiana na wazazi na walimu katika kumlea mtoto.

## 4.0 Malengo ya Elimu ya Awali

Malengo ya Elimu ya Awali ni:

(a) Kujenga misingi imara ya makuzi ya kimwili na uratibu wa misuli mikubwa na midogo;

(b) Kukuza maadili na uwezo wa mtoto kuthamini na kudumisha tunu za taifa na utamaduni wa jamii yake;

(c) Kukuza stadi za awali za lugha na mawasiliano (kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika), Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), mawasiliano mguso, na maandishi ya Breli;

(d) Kukuza stadi za awali za ujifunzaji wa mtoto na tabia ya kupenda kujifunza;

(e) Kujenga uwezo wa mtoto kijamii na kihisia;

(f) Kukuza urazini na ujumi wa mtoto katika kutunza afya na mazingira;

(g) Kukuza stadi za awali za kihisabati, kufikiri kimantiki, kutatua matatizo, ubunifu, uvumbuzi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA);

(h) Kubaini mtoto mwenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki; na

**5.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I na la II**

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I na la II ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya Breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na mawasiliano mguso;

(b) Kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na teknolojia saidizi;

(c) Kujenga uimara wa mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;

(d) Kukuza urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo;

(e) Kukuza maadili na uwezo wa kuthamini na kudumisha tunu za taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali; na

(f) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

**6.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Awali**

Umahiri wa jumla umejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijiti na uzalendo ambao umefafanuliwa katika maeneo ya ujifunzaji kama ifuatavyo:

(a) Utamaduni, Elimu ya Imani, Sanaa na Michezo;
(b) Lugha na Mawasiliano;
(c) Stadi za Awali za Maisha;
(d) Afya na Mazingira; na
(e) Stadi za Awali za Kihisabati, Sayansi na TEHAMA.

**7.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II**

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la I na la II ni:

a) Kutumia stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya Breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na mawasiliano mguso;

b) Kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na teknolojia saidizi;

c) Kushiriki katika vitendo vya kuimarisha mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;

d) Kuonesha urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo;

e) Kuonesha maadili, kuthamini na kudumisha tunu za taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali; na

f) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 8.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Elimu ya Awali

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya awali imebainishwa katika Jedwali Namba 1.

**Jedwali Na. 1 :***Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Elimu ya Awali*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumpenda Allah (*Subhaanahu Wata'ala* na Mtume wake | 1.1 Kumpenda Allah (*Subhaanahu Wata'ala*)<br>1.2 Kumpenda Mtume Muhammad (*Swallallaahu'Alayhi Wasallam* ) |

## 9.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la I na la II

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Darasa la I na la II umebainishwa katika Jedwali Namba 2.

**Jedwali Na.2** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la I na la II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kufuata misingi ya Dini ya Kiislamu. | 1.1 Kumtambua Allah (*Subhaanahu Wata'ala* )<br>1.2 Kutambua nguzo za Uislamu<br>1.3 Kumudu stadi za awali za kusoma Qur'an<br>1.4. Kusoma sura teule<br>1.5 Kuishi kwa kumuiga Nabii Muhammad *(Swallallaahu'Alayhi Wasallam)* |

## 10.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na Ujifunzaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu utazingatia ujenzi wa umahiri unaotumia mbinu zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Mwalimu atatumia mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi. Mwalimu mlezi anashauriwa kuwahusisha watoto katika somo kwa njia ya maelekezo, maswali mafupi pamoja na vitendo.Watoto watumie milango yote ya fahamu: kugusa, kuona, kusikia, kunusa na kuonja. Kwa hiyo, kuna ulazima wa kutumia vitu halisi kama picha na vielelezo vingine katika kuwaelekeza watoto maudhui iliyokusudiwa.

## 11.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji ya umri na uwezo wa mwanafunzi. Mwalimu anapaswa kuhakikisha mwanafunzi anapata nafasi ya kuona, kusikia na kushika zana. Aidha, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwanafunzi kuelewa kinachofundishwa. Mwalimu anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzungumka.

## 12.0 Upimaji

Kwa kawaida mtoto wa darasa la awali hapewi mtihani kama wawavyo wale wa shule ya msingi. Kutakuwa na upimaji wa maendeleo ya mtoto kwa kuangalia uwezo wake. Kazi hii inafanywa kwa kuangalia kumbukumbu za maendeleo ya mtoto tangu alipoanza kuhudhuria elimu ya awali hadi anamaliza. Kwa hiyo, mwalimu anapaswa kuwa na utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu za kila mtoto.

Upimaji wa darasa la I na la II utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kumwezesha mwanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo na zana nyingine kama hizo. Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, mwezi, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathimini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji.

## 13.0 Muda wa Kufundisha

Kwa watoto wa Elimu ya awali, muda wa kila kipindi ni dakika ishirini (20). Mwalimu anaweza kuanza kufundisha umahiri mahususi au shughuli yoyote kulingana na hali ya mazingira na mahitaji ya watoto. Mwalimu anapaswa kutengeneza ratiba itakayoweka uwiano mzuri kwa umahiri mahususi zote na shughuli za ujifunzaji zote 11. Kwa upande wa darasa la I na la II makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji yamewekwa kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kuna vipindi viwili kwa wiki na kila kipindi ni dakika ishirini (20).

**Jedwali Na. 3 :***Mgawanyo wa vipindi kwa Elimu ya Awali*

| | **Umahiri mahususi** | **Na.** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kumpenda Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | 1 | Kutamka majina mazuri mepesi ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala* {Allah, Ar Rahman, Ar Rahiim n.k} | 6 |
| | | 2 | Kumshukuru Allah (*Subhaanahu Wata'ala* kwa kila jambo | 6 |
| | | 3 | Kuwatii wazazi | 4 |
| | | 4 | Kuhifadhi dua na adhkari nyepesi | 8 |
| | | 5 | Kutunza mazingira | 8 |
| | | 6 | Kusikiliza Qur'an | 8 |
| 2 | Kumpenda Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* | 7 | Kutamka majina mazuri ya Mtume (Swallallaahu'Alayhi Wasallam) | 4 |
| | | 8 | Kumswalia Mtume (*Swallallaahu'Alayhi Wasallam)* kila anapotajwa | 6 |
| | | *9* | Kuiga tabia njema alizofundisha Mtume *(Swallallaahu'Alayhi Wasallam)* | 6 |
| | | 10 | Kufanya ibada nyepesi kwa namna alivyofundisha Mtume (*Swallallaahu'Alayhi Wasallam)* | 8 |
| | | 11 | Kuwa na tabia ya usafi | 6 |
| **Jumla ya idadi ya vipindi kwa mwaka** | | | | **70** |

**Jedwali Na. 4:** *Mgawanyo wa vipindi kwa Darasa la I*

| | Umahiri mahususi | Na. | Shughuli za ujifunzaji | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kumtambua Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | 1 | (a) Kueleza sifa ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) ya Kuumba | 4 |
| | | 2 | (b) Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 1-20 | 10 |
| 2 | Kutambua nguzo za Uislamu | 3 | (a) Kubainisha nguzo tano za Uislamu kwa mpangilio | 4 |
| | | 4 | (b) Kutamka shahada | 6 |
| 3 | Kumudu stadi za awali za kusoma Qur'an | 5 | a) Kusoma na kuandika herufi za hijai | 10 |
| | | 6 | b) Kuhusianisha sauti na herufi zenye haraka (shakli) Mfano: *{ بَ→ ba (fat-ha)* <br> *بِ→ bi (kasra)* <br> *بُ→ bu (dhamma)}* | 10 |
| 4 | Kusoma-Sura teule (Fat-ha na Nnaas) | 7 | (a) Kusoma na kutafsiri sura teule (*Fat-ha na Nnaas*) | 10 |
| | | 8 | (b) Kubainisha ujumbe wa sura teule (*Fat-ha na Nnaas*) | 4 |
| 5 | Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* | 9 | (a) Kusalimia na kuitikia salamu ya Kiislamu | 4 |
| | | 10 | (b) Kuiga tabia njema ya Mtume (Swallallaahu'Alayhi Wasallam) {*adabu za kula, kuwa na huruma, upole n.k}* | 4 |
| | | 11 | (c) Kusikiliza kisa kifupi cha kuzaliwa kwa Mtume Muhammad *(Swallallaahu'Alayhi Wasallam)* | 4 |
| **Jumla ya idadi ya vipindi kwa mwaka** | | | | **70** |

**Jedwali Na. 5 :** *Mgawanyo wa vipindi kwa Darasa la II*

| | Umahiri mahususi | Na. | Shughuli za ujifunzaji | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kumtambua Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | 12 | (a) Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 21-40 | 6 |
| | | 13 | (b) Kueleza sifa ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) ya kuruzuku | 4 |
| 2 | Kutambua nguzo za Uislamu | 14 | (a) Kutaja vitu vilivyo najisi | 4 |
| | | 15 | (b) kutia udhu | 4 |
| | | 16 | (c) Kubainisha majina ya swala tano na rakaa zake | 4 |
| 3 | Kumudu stadi za awali za kusoma Qur'an | 17 | (a) Kuunganisha herufi za hijai mbili kuunda silabi | 6 |
| | | 18 | (b) Kuhusianisha sauti na herufi zenye *Tanwiin* | 6 |
| 4 | Kusoma sura teule (Falaq,Ikhlas na Lahab) | 19 | (a) Kusoma na kutafsiri sura teule (Falaq,Ikhlas na Lahab) | 12 |
| | | 20 | (b) Kubanisha ujumbe wa sura teule (falaq,Ikhlas na Lahab) | 4 |
| 5 | Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) | 21 | (a) Kusoma adhkari nyepesi za kila siku (*kuanza kusoma, kupiga chafya, n.k)* | 8 |
| | | 22 | (b kuingia na kukaa msikitini kwa kuzingatia adabu za msikiti | 4 |
| | | 23 | (c) Kubainisha mafunzo kutokana na tabia nzuri ya Mtume Muhammad (*Swallallaahu'Alayhi Wasallam*) | 6 |
| **Jumla ya idadi ya vipindi kwa mwaka** | | | | **68** |

## 14.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangwa katika vipengele saba. Vipengele hivyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa pamoja na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika jedwali Na. 6-8

**Jedwali Na. 6 :** *Maudhui ya Elimu ya Awali*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuipenda Dini ya Kiislamu | 1.1 Kumpenda Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* | a)Kutamka majina mazuri mepesi ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala) (Ar Rahman, Ar Rahiim* n.k) | **Onesho mbinu:** Tamka majina ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* kwa sauti kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, (**matamshi sahihi**). Kisha waongoze wanafunzi kutamka | Kutamka majina mazuri mepesi ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala) Ar Rahman, Ar Rahiim* n.k) Kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHA-MA<br>Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHA-MA | 40 |
| | | (b) Kum-shukuru Allah (*Sub-haanahu Wata'ala)* kwa kila jambo (*Bis-millah* - kila anapoanza kufanya kitu *Al-ham-dulilah* - kila anap-omaliza kufanya kitu *Subhaanal-lah* -kila anapopata jambo la kushtusha. | **Michezo:** Kuwaongo-za wanafun-zi katika mistari miwili kwa kubadilisha-na kucheza michezo. Mfano "si-mama-kaa" huku wakitamka maneno: *Bismilallh, Alham-dulilah* na *subhannal-lah*) | Kumshukuru (Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) kwa kila jambo *(Bismillah* -kila anapoanza kufanya kitu *Al-hamdulilah* -kila anapomaliza kufanya kitu *Subhaanallah* - kila anapopata jambo la kushtusha kumefanyika | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kutunza mazingira (kutupa takataka sehemu sahihi na kutowatesa viumbe- kuonyesha upendo kwa Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) kupitia kutunza alichokiumba) | **Ziara:** Waelekeze wanafunzi kwenda kutembea katika mazingira ya shule na kuokota takataka na kuzipeleka sehemu husika. Pia, waelekeze watakapomuona mdudu asiye na madhara wamuache aende zake. | Mazingira yametunzwa | | |
| | | (f) Kusikiliza Qur'an | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza Qur'an kwenye kifaa cha TEHAMA huku ukiwahimiza kuwa watulivu. | Qur'an imesikilizwa | | |
| | 1.2 Kumpenda Mtume Muhammad (*Swallallah alayhi wa sallam*) | (a) Kutamka majina mazuri ya Mtume (mfano: *Muhammad, As Siddiq, Al amin*) | **Onesho mbinu:** Soma kwa sauti kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, (matamshi sahihi) Kisha waongoze wanafunzi kutamka kwa kufuatisha | Majina mazuri ya Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*) yametamkwa | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA | 32 |
| | | (b)Kumswalia Mtume (*Swallallah alayhi wa slaam*) kila anapotajwa (*Swallallah alayhi wasallam*) | **Onesho mbinu:** Soma kwa sauti kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, (matamshi sahihi) Kisha waongoze wanafunzi kutamka kwa kufuatisha | Kila alipotajwa Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*), ameswaliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuiga tabia njema alizofundisha Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*) {mfano: kusema ukweli, kuwa na heshima, kupanga vitu vizuri, kuwa na huruma, kula kwa mkono wa kulia, n.k} | **Hadithi:** Simulia hadithi kuhusu mtoto mwenye tabia njema kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti. Kisha waongoze wanafunzi kutaja sifa nzuri kwa kuzingatia hadithi waliyosikiliza. | Kuiga tabia njema alizofundisha Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*) kumefanyika | | |
| | | (d) Kufanya ibada nyepesi kwa namna alivyofundisha Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*) {mfano: kusimama vizuri katika swala} | **Onesho Mbinu:** Wagawe wanafunzi na kuwapanga katika mistari na kuwaelekeza namna ya kusimama kwa kunyosha mistari | Kufanya ibada nyepasi kwa namna alivyofundisha Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*) kumefanyika | | |
| | | (e) Kuwa na tabia ya usafi (Mtume alipenda sana usafi, hivyo mtoto akionesha usafi wa mwili, nguo na sehemu yake ya kucheza ni dalili ya kumpenda Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*) | **Hadithi**: Simulia hadithi kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti kuhusu maisha ya Mtume Muhammad (*Swallallah alayhi wasallam*) kama alivyokuwa msafi, kisha waongoze wanafunzi wataje tabia nzuri za Mtume (*Swallallah alayhi wasallam*) | Tabia ya usafi imeonekana | | |

**Jedwali Na. 7:** *Maudhui ya Darasa la I*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahsusi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifun- zaji zinazo- pendekez- wa | Idadi ya vip- indi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kufuata misingi ya Dini ya Kiislamu. | 1.1 Kutambua nguzo za Uislamu | (a) Kubainisha nguzo tano za Uislamu kwa mpangilio | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kutokana na matini waliyosoma | Kubainisha nguzo tano za Uislamu kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | **10** |
| | | (b) Kutamka shahada | **Onesho mbinu:** Waongoze wanafunzi kutamka Shahada kwa kufuatisha kisha waongoze kutamka shahada hiyo | Kutamka shahada kumefanyika | | |
| | 1.2 Kumtam- bua Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | (a) Kueleza sifa ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) ya Kuumba | **Picha na maelezo:** Onesha picha mbalimbali zinazobainisha viumbe vya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) mfano Mlima, Jua, kisha eleza utukufu wa Allah katika kuumba | Sifa ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) ya kuumba imeelezwa | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 14 |
| | | (b) Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 1-20 | **Onesho mbinu:** Waoneshe video ya utamkaji wa sauti za herufi za hijai kisha Waongoze wanafunzi kutamka sauti za herufi za hijai kufuatisha unavyotamka na inavyoonekana kwenye video | Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 1-20 kumefanyika | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo- pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 Kumudu stadi za awali ya kusoma Qur'an | a) Kusoma na kuandika herufi za hijai | **Onesho mbinu:** Waongoze wanafunzi kutamka sauti za herufi za hijai kufuatisha unavyotamka na uwaoneshe video ya utamkaji wa sauti za herufi za hijai kisha waongoze kutamka sauti za herufi hizo | Kusoma na kuandika herufi za hijai kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 20 |
| | | b) Kuhusianisha sauti na herufi zenye haraka (*shakli*) Mfano: {بَ → ba *(fat-ha)* بِ → bi (*kasra*)\ ب → bu (*dhamma*)} | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza utamkaji wa herufi za hijai zenye haraka kupitia kifaa cha TEHAMA kisha waelekeze watamke | kuhusianisha sauti na herufi zenye haraka kumefanyika | | |
| | 1.4 Kusoma sura teule (*Fat-ha* na *Nnaas*) | (a) Kusoma na kutafsiri sura teule (*Fat-ha* na *Nnaas*) | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza usomaji wa sura teule kwa kutumia kifaa cha TEHAMA kisha waelekeze wasome. | Kusoma na kutafsiri sura teule (Fat-ha na Nnaas) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 14 |
| | | (b) Kubainisha ujumbe wa sura teule (*Fat-ha* na *Nnaas*) | **Majadiliano**: waongoze wanafunzi kusoma matini juu ya tafsiri ya sura teule kisha kujadiliana kwa kutumia matini | Kubainisha ujumbe wa sura teule *(Fat-ha* na *Nnaas*) kumefanyika | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.5 Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) | (a) Kusalimia na kuitikia salamu ya Kiislamu | **Bakuli la Samaki:** Waongoze wanafunzi kukaa katika maduara mawili (duara la ndani na duara la nje) kisha wale wa ndani wasalimie na wa nje waitikie kisha wabadilishane. Zoezi lirudiwe mara tatu. | Kusalimia na kuitikia salamu ya Kiislamu kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 12 |
| | | (b) Kuiga tabia njema ya Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) {adabu za kula, huruma, upole n.k} | **Picha na maelezo:** Onesha picha za watoto wanakula kwa adabu kisha toa maelezo<br><br>**Igizo:** Waongoze wanafunzi kuigiza tabia njema (kula kwa adabu n.k) | Kuiga tabia njema ya Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) {adabu za kula, huruma, upole kumefanyika | | |
| | | (c) Kusikiliza kisa kifupi cha kuzaliwa Mtume Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza kisa kilichotokea wakati anazaliwa Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) kisha waulize maswali kutokana na masimulizi hayo. | Kusikiliza kisa kifupi cha kuzaliwa Mtume Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | |

**Jedwali Na.8** *Maudhui ya Darasa la II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahsusi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kufuata misingi ya Dini ya Kiislamu. | 1.1 Kumtambua Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | (a) Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) (21-40) | **Picha na maelezo:** Onesha picha za maiina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*), kisha kwa njia ya kasida/ nashidi waongoze wanafunzi wataje majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) (21-40) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 10 |
| | | (b) Kueleza sifa ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) ya kuruzuku | **Onesho mbinu:** Waoneshe wanafunzi picha za viumbe hai vikipata riziki: (watu, wadudu, wanyama wa porini na mifugo n.k) kisha waulize maswali ya tafakuri. | Kueleza sifa ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) ya kuruzuku kumefanyika | | |
| | 1.2 Kufafanua nguzo za Uislamu | (a) Kutaja vitu vilivyo najisi | **Picha na maelezo:** Onesha picha zinazobainisha vitu vilivyo najisi, kisha taja majina ya vitu hivyo | Kutaja vitu vilivyo najisi kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 12 |
| | | (b) Kutia udhu | **Onesho mbinu:** waoneshe wanafunzi picha zilizo katika mfuatano wa mtu anayetia udhu ,uwaongoze kutambua kila kitendo katika picha hizo. | Kutia udhu kumefanyika | | |
| | | | **Igizo:** waongoze wanafunzi kuigiza kutia udhu hatua kwa hatua | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kubainisha majina ya swala tano na rakaa zake | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kutokana na matini waliyosoma | Kubainisha majina ya swala tano na rakaa zake kumefanyika | | |
| | 1.3 Kumudu stadi za awali za kusoma Qur'an | (a) Kuunganisha herufi za hijai mbili kuunda silabi | **Uchambuzi wa matini:** waongoze wanafunzi kusoma matini zenye sauti za silabi zenye herufi mbili wabainishe herufi hizo | Kuunganisha herufi za hijai mbili kuunda silabi) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 14 |
| | | (b) Kuhusianisha sauti na herufi zenye Tanwiin: mfano:<br>بً → ban (*fat-hatain*)<br>بٍ→ bin (*kasratain*)<br>بٌ→ bun (*dhammatain* | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye herufi zenye *tanwiin* wabainishe *tanwiin* hizo | Sauti na herufi zenye tanwiin vimehusia-nishwa | | |
| | 1.4 Kusoma Sura teule (*Falaq, Ikhlas* na *Lahab*) | (a) Kusoma na kutafsiri sura teule (*Falaq, Ikhlas* na *Lahab*) | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza usomaji wa sura teule kupitia kifaa cha TEHAMA kisha waelekeze wasome. | Kusoma na kutafsiri sura teule (*Falaq*, -*Ikhlas* na *Lahab*) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 16 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazope - ndekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubanisha ujumbe wa sura teule (*Falaq, Ikhlas* na *Lahab*) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusoma matini juu ya tafsiri ya sura teule kisha kujadiliana kwa kutumia matini umuhimu wa kujikinga kwa Mola Mlezi kutokana na shari za usiku, hasadi, wachawi Pia kujiepusha na kiburi | ujumbe wa sura teule (*Falaq, Ikhlas* na *Lahab*) umebainishwa | | |
| | 1.5 Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) | (a) Kusoma adhkari nyepesi za matukio mfano; kupiga chafya, kula, n.k) | **Onesho mbinu:** Waongoze wanafunzi kutamka adhkari za kila siku kufuatisha unayotamka na waoneshe video ya utamkaji wa adhkari, kisha waongoze kutamka adhkari hizo. | Kusoma adhkari nyepesi za matukio mfano;kupiga chafya, kula n.k) Kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi | 18 |
| | | (b) Kuingia na kukaa msikitini kwa kuzingatia adabu za msikitini | **Igizo:** Waongoze wanafunzi waigize kuingia msikitini kwa kuzingatia adabu za msikitini. | Kuingia na kukaa msikitini kwa kuzingatia adabu za msikitini kumefanyika | | |
| | | (c) Kubainisha mafunzo kutokana na tabia nzuri ya Mtume Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) | **Masimulizi**: Simulia tabia ya Mtume Muhammad (Swallallaahu 'Alayhi Wasallam) Kisha waongoze wanafunzi wahusishe tabia hizo na hali halisi ya maisha yao. | Kubainisha mafunzo kutokana na tabia nzuri ya Mtume Muhmamad (Swallallaahu 'Alayhi . Wasallam) kumefanyika | | |

## Bibliografia

Islamic Education Panel (IEP) (2012). *Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu,Elimu ya Msingi Darasa la 1-VII*

Islamic Education Panel (IEP) (2012). *Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu,Elimu ya Awali.IEP*

Taasisi ya Elimu Tanzania (2023). *Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali.Taasisi ya Elimu Tanzania.*

Taasisi ya Elimu Tanzania (2023). *Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa La I-II.* Taasisi ya Elimu Tanzania